

## KITENDEA KAZI CHA MHUDUMU WA AFYA YA UZAZI NA MTOTO KATIKA JAMII NA MTEJA

**Uhusiano kati ya matumizi ya sindano katika kupanga uzazi na kuongezeka kwa uwezekano wa kuambukizwa VVU**

### Je kuna uhusiano gani ?

- Kuna taarifa za uwezekano kwa kuongezeka kwa uwezekano wa kuambukizwa VVU kwa wanawake wanaotumia njia ya sindano katika kupanga uzazi.
- Baadhi ya tafiti zimeonyesha kuwa wanawake wanaotumia njia ya sindano huwa katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU, ukilinganisha na wasiotumia njia hii.
- Hata hivyo taarifa hizi hazina ushahidi wa kutosha na tafiti zaidi zinaendelea ili kupata majibu sahihi yenye ushahidi wa kutosha ikiwa kama sindano husababi sha kuongezeka kwa uwezekano huo au la.

### Unatakiwa kutoa ushauri gani?

- Njia ya sindano ni salama na inaweza kutumika na wanawake wote. Hata hivyo, kuna taarifa kuwa njia hii inaweza kuongeza uwezekano wa kuambukizwa VVU
- Mwanamke anayetaka kutumia njia hii, ashauriwe kufikiri zaidi kuhusu maisha yake na athari zitokanazo na mimba zisizotarajiwa, kama vile magonjwa na vifo kwa wajawazito na watoto, ukilinganisha na uwezekano wa kupata maambukizi na kumuambukiza mwanao. Ni vizuri kufanya chagua sahihi kwa maisha yako
- Kuna njia nyingine za uzazi wa mpango ambazo mwanamke anayehisi yuko katika hatari ya maambukizi ya VVU na asingependa kuchagua njia ya sindano, anaweza kutumia. Njia za uzazi wa mpango kama vipangikizi, vidonge vyewe vichocheo viwili (COC) ni nzuri na zinafanya kazi vizuri katika kuzuia mimba zisi zotarajiwa ikiwa zitatumika kwa usahihi na kila wakati
- Mwanamke anao uhuru wa kuchagua njia ya uzazi wa mpango inayomfaa zaidi. Mtoa huduma anapaswa kumpa ushauri wa faida na hasara za njia zote zinazo patika

### Kumbuka

- Njia za uzazi wa mpango kama vipangikizi, vidonge vyewe vichocheo viwili, sindano na kondomu zinafanya kazi vizuri katika kuzuia mimba zisizotarajiwa ikiwa zitatumika kwa usahihi na kila wakati.
- Ni vizuri kutumia condom pia ikiwa unahisi uko katika hatari ya kupata maambukizi ya VVU au magonjwa ya zinaa
- Ni vizuri kutumia kondom ili itoe kinga mara mbili (dual protection) kwa maana ya kutumia kondom pamoja na njia nyingine ya uzazi wa mpango kutasaidi kuzuia mimba zisizotarajiwa na pia maambukizi ya VVU na magonjwa ya zinaa